



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI
(NACTE)



TAARIFA KWA UMMA

MATOKEO YA UCHAGUZI WA AWAMU YA PILI WA PROGRAMU MBALIMBALI
ZINAZOTOLEWA NA VYUO VYA UFUNDI KWA MKUPUO WA SEPTEMBER KWA
MWAKA WA MASOMO 2021/2022

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ni chombo kilichoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Sura ya 129, ili kusimamia na kuratibu utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi katika vyuo vya Elimu ya Ufundi hapa nchini. Jukumu mojawapo la Baraza ni kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa katika Vyuo vya Ufundi nchini yanakidhi vigezo na ubora unaohitajika katika soko la ajira ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Baraza linao wajibu wa kuratibu udahili wa wanafunzi kwenye vyuo na kozi/programu zinazotambulika na mamlaka husika.

Baraza linataarifu umma kwamba limekamilisha uhakiki wa waombaji waliochaguliwa na Vyuo na Taasisi mbalimbali katika Awamu ya Pili. Katika awamu hii jumla ya waombaji **24,303** walichaguliwa na Vyuo na Taasisi mbalimbali zinazotoa mafunzo katika ngazi ya Cheti na Stashahada. Baada ya kukamilika kwa uhakiki, imebainika kwamba jumla ya waombaji **22,278** waliokuwa wamechaguliwa na Vyuo na Taasisi mbalimbali wana sifa za kujiunga na kusoma kozi walizochaguliwa. Aidha, jumla ya waombaji **2,025** waliochaguliwa na Vyuo/Taasisi hawakuwa na sifa za kujiunga na kusoma kozi walizochaguliwa. Baraza limebaini kuwa kati ya waombaji waliokosa sifa imetokana na Vyuo/Taasisi kuwawasilisha majina ya waombaji kwenye kozi zisizo sahihi, taarifa pungufu kwa wanafunzi waliorudia mitihani ya Kidato cha Nne zaidi ya mara moja, viambatanisho vya vyeti kukosekana (transcripts and certificates) na kukosewa kwa namba za usajili za Astashahada Msingi na Astashahada zilizo kwenye kanzidata ya Baraza.

Baraza limeongeza siku tano (5) zingine za ziada kuanzia tarehe **15 hadi 19 Oktoba, 2021** kwa Wakuu wa Vyuo vyote vilivyopokea wanafunzi hao, isipokuwa vile vya Afya vya Serikali kuwasilisha majina hayo kupitia tovuti ya NACTE (www.nacte.go.tz). Vyuo hivyo vitaruhusiwa kusajili wanafunzi hao baada ya kuhakikiwa. Hivyo, Vyuo, isipokuwa vile vya Afya vya Serikali, vinashauriwa kurekebisha taarifa hizo na kutumia fursa hiyo kuwasilisha majina ya waombaji waliochaguliwa na kushindwa kuwawasilisha kutoka Dirisha la Kwanza na la Pili la Uhakiki.

Vyuo vya Serikali, isipokuwa vile vya Afya vya Serikali vilivyopokea wanafunzi waliopangiwa masomo na Ofisi ya Rais - TAMISEMI vinaelekezwa kuandaa maombi yao na kuwasilisha majina ya wanafunzi ambao hawakuthibisisha kwa ajili ya uhakiki. Majibu ya uhakiki yatatolewa tarehe **25 Oktoba, 2021**. Aidha, Baraza limevielekeza kwa barua, Vyuo vya Afya vya Serikali vyenye nafasi tu, namna ya kuwapokea wanafunzi hao ambao hawakuthibitisha kuanzia tarehe **19 Oktoba 2021**.

Baraza linaendelea kutoa wito kwa Vyuo na Taasisi zinazotoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada na Stashahada kuhakikisha kwamba wanafunzi wanaosajiliwa kwa ajili ya masomo ni wale tu walio na sifa baada uhakiki kufanywa na Baraza.

Usajili kwa wanafunzi waliofika chuoni kwa mwaka wa masomo 2021/2022 utanza rasmi tarehe **18 Oktoba, 2021** kama ilivyo kwenye Kalenda ya Matukio Muhimu ya Kitaaluma inayopatika kwenye tovuti ya Baraza (www.nacte.go.tz).

IMETOLEWA NA:
OFISI YA KATIBU MTENDAJI
BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI (NACTE)
TAREHE: 15/10/2021